*Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 1-17*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Uhusiano Baina ya Silika na Utendaji wa Wahusika Wakuu wa Fasihi ya Watoto

*Saumu Kabanda Mkomwa*[1]

## Ikisiri

Makala hii inahusu uhusiano baina ya silika na utendaji wa wahusika wakuu wa fasihi ya watoto kwa kurejelea riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*. Data za msingi zilizotumika katika makala hii zilipatikana maktabani kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Nadharia ya Saikochanganuzi imetumika katika ufafanuzi huo, ambayo iliasisiwa na mwanasaikolojia wa Kiswisi Sigmund Freud (1856-1939). Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kila mhusika ana silika yake yenye sifa zinazomtofautisha na mhusika mwingine. Silika humsukuma mhusika kutenda mambo mbalimbali ambayo yanaweza kuwa hasi au chanya. Hakuna silika bora kuliko nyingine, zote zipo ili kuifanya dunia iwe mahali salama pa kuishi. Mtafiti anaamini kuwa makala hii itakuwa chachu kwa waandishi na watunzi kutunga kazi zitakazoendana na silika za watoto, hivyo, zitakuwa rahisi kueleweka kwa watoto ambao ndio walengwa wakuu. Makala inahitimisha kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya silika na utendaji kwani dhana hizi zinaathiriana na kukamilishana. Silika ndiyo humsukuma mhusika kutenda jambo fulani na huwezi kugundua silika ya mhusika kama hajatenda jambo hilo.

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya watoto, kama zilivyo aina nyingine, hutegemea wahusika kama msingi muhimu katika matukio yanayoisukuma hadithi tangu mwanzo hadi mwisho. Wahusika hukusudiwa wawasilishe dhana, fikra au tabia za watu (Mbunda, 1993). Wahusika wakuu ndio wanaobeba mawazo ambayo mwandishi hudhamiria kuyapeleka kwa hadhira husika. Maudhui ya kazi ya fasihi huwa yanamzungukia na hata kutolewa na mhusika huyo zaidi kuliko wahusika wengine. Hivyo, wahusika wamekuwa midomo na vipaza sauti vya watunzi (Senkoro, 2011). Mhakiki na mtafiti wanalazimika kuuelewa uhusika wa kila mhusika katika kazi ya fasihi. Wahusika wanaweza kuumbwa kinafsi, kiakili na kimwili. Ujenzi huu wa kinafsi na kimwili huonesha wasifu wake wa ndani na nje au anaweza kuonesha mabadiliko yake kila anapokutana na hali isiyo ya kawaida. Mabadiliko haya huathiriwa na nguvu za kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi (Muhando na Balisidya, 1976). Katika ujenzi huo wahusika hutenda mambo mbalimbali ili kusukuma mbele maudhui yaliyodhamiriwa na mwandishi. Wahusika wengine huthubutu kufanya mambo ya hatari ambayo hayaendani na jinsi na umri wao. Kwa mujibu wa Mudhihiri (2019) mambo hayo ni silika inayomsukuma mtu kuutawala ulimwengu.

---

[1] Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Fedha za Maendeleo na Mafunzo ya Uongozi, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP), Dodoma, Tanzania. Baruapepe: saumumkomwa77@gmail.com

Kwa mujibu wa makala hii, silika ni maumbile ya msingi ya kihaiba ambayo mtu huzaliwa nayo. Maumbile haya ni ya kidhahania kwani hayawezi kuonekana hadi mtu atende jambo, ndipo husemwa ana silika fulani. Ponera na Kasiga (2019) wanaifafanua silika kama vionjo vya kihaiba ambavyo ni asili ya tabia au hali ya mtu aliyozaliwa nayo. Mara nyingi silika huwa haibadiliki bali huimarishwa au kudhoofishwa na malezi, elimu na jamii inayomzunguka mtu. Kwa upande mwingine utendaji ni ufanyaji wa jambo. Hii inajumuisha namna jambo linavyofanyika, eneo lilipofanyika na nani aliyelifanya (Mlaga, 2017). Makala hii inafafanua utendaji kama uwasilishaji wa tukio kwa lugha ya mazungumzo baina ya wahusika na masimulizi ya kiutendaji yanayokwenda sambamba na mazungumzo hayo. Ili kuzisoma na kuzielewa kazi zilizoandaliwa kwa ajili ya watoto, makala hii imeona umuhimu wa kuzifahamu silika za wahusika wakuu katika riwaya teule na kuzihusianisha na utendaji wao. Hii ni kwa sababu kwa kuzijua silika inaaminiwa kwamba waandishi watatunga kazi zinazoendana na silika za watoto. Kwa hiyo, watoto watazisoma na kujinasibisha na wahusika hao, hivyo, kuwa miongoni mwao na kufuatilia hadithi kwa umakini. Kwa kufanya hivyo, mtafiti anaamini watazielewa hadithi zilizotungwa au kusimuliwa kwa ajili yao. Wanasaikolojia wanazibainisha silika katika makundi makuu mawili ambayo nayo hugawanyika katika makundi mawilimawili, hivyo, kuwa na aina nne za silika (Martine na Bobgan, 1992; Larrimore, 2001; Flaskerud, 2012; Asamoah, 2018). Makundi hayo na sifa zake yanaoneshwa katika Jedwali Na. 1 lifuatalo:

**Jedwali Na. 1: Mgawanyo wa Aina za Silika na Sifa zake**

| **Sifa za Utu** | **Wasondani *(extroverts)*** | | **Wandani *(introverts)*** | |
|---|---|---|---|---|
| **Aina za Silika** | **Sangwini** | **Koleriki** | **Melankoli** | **Flegmatiki** |
| **Sifa za Silika** | Mchangamfu | Hujiona bora kuliko wengine | Msikivu | Mtulivu |
| | Rafiki | Ana fujo | Mchambuzi wa mambo | Mfanisi |
| | Muongeaji | Ana ushawishi | Ana hasira za karibu | Tegemezi |
| | Mbinafsi | Anajiamini | Mtafutaji | Anaingilika kirahisi |
| | Siyo tegemezi | Mwenye nguvu | Hujiona mkamilifu | Siyo mzungumzaji |
| | Hakai mahali pamoja | Ana hasira za haraka | Hajichanganyi na watu au kuungana | Mvivu |
| | Huonekana sana popote alipo | Anapuuza mambo | Ni mgumu kubadilika | mkaidi |

**Chanzo:** Mtafiti (2020) imeboreshwa kutoka Martin na Bobgan (1992)

Makala hii ina sehemu kuu sita ambazo ni: utangulizi ambao umeshughulikia dhana za msingi zilizotumika katika makala hii na kufafanua lengo la makala; muhtasari wa riwaya teule ambapo riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* imeelezewa kwa ufupi; ufafanuzi wa kiunzi cha nadharia kilichotumika katika mchakato mzima wa utafiti; methodolojia ambayo imeeleza mbinu iliyotumika kuchagua riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*, silika za wahusika wakuu katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* ambapo sehemu hii imefafanua silika za kila mhusika kutokana na matendo yake, na hitimisho lililoeleza kwa ufupi yale yaliyojadiliwa katika makala nzima pamoja na tija itakayopatikana kutokana na makala hii.

## 2.0 Muhtasari wa Riwaya Teule

Riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* ni ya kihistoria ya mapambano ya Wahehe na Wasagara dhidi ya Wadachi, mwaka 1891. Riwaya hii ilitolewa kwa mara ya kwanza mwaka 1991, kisha chapa hii ya mwaka 2018. Riwaya hii iliyotungwa na Mugyabuso Mlinzi Mulokozi inasimulia masahibu yaliyowakuta Mbumi na Chulu katika safari yao ya kuelekea Iringa kupeleka ujumbe wa siri wa mbiu ya mapambano kwa Mutwa Mukwava (Mkwawa) baada ya Wadachi kuivamia Usagara na kuanza kuinyemelea Uhehe. Vijana hawa ni pacha wenye umri wa miaka kumi na sita. Baadhi ya masahibu yanayowakumba ni pamoja na kutembea mwendo mrefu katika milima, mabonde na vichaka vikubwa. Pia, wanashuhudia vifo vya ndugu zao na vya Wadachi ambao walivamia Usagara. Katika mapambano dhidi ya Wadachi, wanafanikiwa kumkamata mateka mmoja, pia kumuua Nyundo, Jemadari wa Wadachi kwa kushirikiana na Mpunza[2]. Hatimaye, wanafanikiwa kuwasilisha ujumbe wao wa haraka kwa Mutwa na kutangazwa kuwa mashujaa.

## 3.0 Kiunzi cha Nadharia

Data za makala hii zimechambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Saikochanganuzi. Kwa mujibu wa Mulokozi (2017) saikochanganuzi huibua hisia na silika zilizozimwa kutoka katika ung'amuzibwete (*unconsciousness*) kuingia katika hali ya umaizi (*consciousness*). Katika fasihi, hisia na silika hizo huweza kumhusu mwandishi au wahusika wake. Nadharia hii iliasisiwa na mwanasaikolojia wa Kiswisi, Sigmund Freud (1856-1939). Kwa mtazamo wa Freud, lugha huakisi michakato ya akilini inayojibainisha katika ndoto, misemo na usemaji. Aidha, amebainisha nafsi tatu; nafsi ya kiwango cha msingi (*Id)* ambayo ni nafsi ya kisilika na matamanio bila urazini, hali ya unyama, kitovu cha misukumo ya kisilika kama ushari na ashiki dhidi ya dhamiri. Pili, nafsi ya kiwango cha kati *(Ego)* ambayo ni nafsi ya utashi, urazini na tafakuri inayoongoza maamuzi ya busara, na tatu, nafsi ya kiwango cha ukomavu (*Super-ego)* ambayo ni nafsi ya kidhamira, ya kimaadili, inayochunguza uadilifu wa tendo, wema na ubaya wake, kabla ya kulitenda (Mbarouk, 2009).

Misingi mikuu ya nadharia hii ni mitatu; mahitaji, matamanio na wasiwasi. Kati ya mambo haya matatu, nafasi kubwa huchukuliwa na matamanio. Kwa hiyo, kila binadamu hufanya jitihada kuhakikisha anakamilisha matamanio yake (Wamitila, 2002). Mawazo na matamanio yaliyopo katika akili za binadamu hujitokeza katika nafsi tatu ambazo ni: nafsi ya kiwango cha msingi, nafsi ya kiwango cha kati, na nafsi ya kiwango cha ukomavu. Makala hii imetumia misingi hii katika kuzibainisha aina za silika za wahusika wakuu na kuzihusianisha na utendaji wao. Matamanio humfanya mhusika kutenda kadiri ya mazingira, hivyo, silika yake hutambulika kwa urahisi. Pia, matendo yote ya mhusika huongozwa na nafsi tatu za Freud.

---

[2] Mtoto wa kiume wa Munzagila, makamo ya Chulu, ambaye alikuwa na tembe lake walilolala Mbumi na Chulu baada ya kufika kwao.

## 4.0 Methodolojia

Makala hii imeonesha uhusiano baina ya silika na utendaji wa wahusika wakuu wa fasihi ya watoto kwa kurejelea katika riwaya teule. Ili kufikia lengo la makala hii, uchunguzi ulifanyika kwa kusoma maandiko mbalimbali ili kupata taarifa zilizohitajika. Pia, uchunguzi kifani ulitumika kuteua riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* kama matini ya msingi. Creswell (2009) anafafanua uchunguzi kifani kuwa ni uchambuzi wa kina wa tatizo moja. Riwaya hii iliteuliwa kwa sababu ina data za kutosha zilizohitajika kukamilisha lengo la makala. Pia, kutokana na mawanda ya utafiti yaliyozalisha makala hii, riwaya moja imetosha kupata data zilizohitajika. Katika uchambuzi wa data, makala imetumia mkabala wa kitaamuli. Mkabala huu hutumiwa kuchambua data kwa mfumo wa maelezo pasipo kufuata utaratibu wa kitakwimu (Kothari, 2004). Sehemu inayofuata inajadili silika za wahusika wakuu katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*.

## 5.0 Silika za Wahusika Wakuu wa Fasihi ya Watoto katika Riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*

Kwa mujibu wa Flaskerud (2012) kila mtu ana chembechembe za aina nne za silika ndani mwake, japo moja hujitokeza zaidi na kufuatiwa na nyingine. Kutokana na ujitokezaji huo wa aina mojawapo ya silika ndipo inasemwa fulani ana silika za aina hii au ile. Kwa hiyo, hakuna mtu anayemiliki aina moja ya silika, bali wengi wanayo moja yenye nguvu kuliko nyingine. Hili pia linajitokeza kwa wahusika ambao ni wawakilishi wa binadamu. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, ilibainika kuwa kila mhusika ana silika yake ambayo humtofautisha na mhusika mwingine kutokana na utendaji wao. Zifuatazo ni aina za silika za wahusika wakuu wa fasihi ya watoto katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*.

### 5.1 Silika ya Chulu

Huyu ni pacha wa kiume ambaye mwandishi amemsawiri kwa kumpa matendo yanayomuweka katika silika ya melankoli. Silika hii ipo katika kundi la wandani ambao wana uwezo mkubwa kiakili. Sifa za silika hii kwa mujibu wa mhusika huyu ni kama ifuatavyo: kwanza ni watu wanaofuata sheria na taratibu. Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa Chulu ni mfuasi mkubwa wa sheria na taratibu; zinaweza kuwa za nchi au za jamii fulani ambazo hutofautiana na jamii nyingine. Taratibu hizi zinaweza kuwa mila na desturi za jamii husika. Katika jamii yao kuna kazi ambazo hufanywa na wanawake na wanaume. Mtoto anapozaliwa huzikuta hivyo, naye anapokua anaendelea kuzifuata. Mathalani, Chulu na Mbumi katika safari yao; siku ya nne walijikuta wako porini na jua limezama, hivyo, ilibidi wapumzike hadi kupambazuke. Ili kujilinda na wanyama wakali ilibidi wawashe moto lakini mwanzoni Chulu aliweka pingamizi juu ya kumsaidia dada yake kutafuta kuni. Mwandishi anafafanua:

> Mbumi alianza kukusanya kuni kavu kutoka katika vichaka vilivyokuwa karibu. Chulu alibaki chini ya mti amejiegemeza kwenye mkuki wake aliousimika ardhini. “Hunisaidii Chulu?” Mbumi alisema.
> “Mwanamume kuchanja kuni si mila yetu,” Chulu alisema.

> "Mambo ya mila yangesubiri tumalize matatizo kwanza; hatuna muda," Mbumi alisema. "Hebu kanisaidie kukata tawi hilo hapo kwenye kichaka kile" (kur. 29-30).

Kwa mujibu wa data zilizopatikana, imedhihirika kuwa taratibu ambazo Chulu anazifuata ni mfumo dume kwa kuwa akilini mwake ametenga kazi za wanawake na wanaume. Hata hivyo, baada ya kuombwa na dada yake anaamua kutupilia mbali mila hizo kutokana na matatizo waliyokuwa nayo, hivyo, anamsaidia dada yake kukata kuni. Kwa mujibu wa nadharia iliyotumika, Chulu anaongozwa na nafsi ya kiwango cha kati kutupilia mbali taratibu hizo na kumsaidia dada yake. Anachunguza wema na ubaya wa tendo hilo kabla ya kulitenda. Kwa hiyo, anaona kuwa si vema kumuacha dada yake kufanya kazi hiyo peke yake wakati ni kwa faida ya wote.

Sehemu nyingine inayoonesha kuwa Chulu ni mtu wa kufuata sheria na taratibu ni pale wanapokubaliana kulala kwa zamu wakiwa porini. Makubaliano hayo yanamtaka aliyeko macho kuhakikisha kuwa moto hauzimiki kwa kuuchochea na kuongeza kuni. Inaanza zamu ya Mbumi kisha inafuata ya Chulu. Katika safari yao, tangu wanapoianza, Chulu amebeba mkuki. Unapofika muda wake wa kulala hataki kupokelewa mkuki huo. Masimulizi yanafafanua:

> Moto uliwaka usiku kucha. Walipokezana kulala na kuchochea moto hadi asubuhi. Zamu ya Chulu ya kulala ilipofika, alikwenda kulala akiwa ameushikilia mkuki wake. Mbumi alimshauri ampokee huo mkuki, lakini Chulu alikataa na kusema kuwa ni muhali kabisa kwa mwanamke kushika mkuki. Alimshauri ashikilie kisu chake tu. Mara mbili tatu mafisi na wanyama wengine wa pori waliwasogelea kwa udadisi, lakini hawakuja karibu sana kwa kuogopa moto (uk. 32).

Inaaminiwa kuwa huo ndio msimamo wa Chulu mara zote anapoona mila na taratibu zinataka kubanangwa. Haya ni maamuzi ya busara lakini kutokana na mazingira waliyo nayo, anatakiwa atupilie mbali mila hizo potofu. Chulu anaruhusu nafsi ya kiwango cha msingi ifanye kazi bila ya kuwa na urazini.

Pili, ni uvumilivu. Watu wa kundi hili ni wavumilivu sana hata wanapokumbwa na mikasa mbalimbali, hatimaye, hufikia mwisho ambao huwa mzuri. Chulu anavumilia sana kutoka mwanzo hadi mwisho wa safari yao. Pamoja na umbali mkubwa wa kutembea, bado anakuwa imara kuliendea lile waliloagizwa[3]. Wanatembea kwa zaidi ya siku tano. Mwandishi anatanabahisha:

> Kwa siku tatu za kwanza hali ilikuwa hivyo. Bali siku ya nne walijikuta bado wapo porini saa za magharibi. Hapakuwa na kijiji chochote karibu. Ilibidi wasimamishe safari yao na kupiga kambi chini ya mti mkubwa wa mgudu… Siku ya tano walianza kuona mabadiliko makubwa zaidi. Milima iliongezeka, baridi iliongezeka, ukungu ulitanda kila asubuhi, na umande baridi ulilowanisha miguu yao… siku ya sita walilala katika

[3] Waliagizwa kupeleka majibu ya ujumbe wa urafiki kwenda kwa Mutwa Mukwava (Mkwawa) Mfalme wa Uhehe pamoja na kumtahadharisha kuhusu maadui (Wadachi). Aliyewaagiza alikuwa Mundewa (Mtemi wa jadi).

> kijiji cha Iringa, karibu na Kalenga… siku iliyofuata, Chulu na Mbumi walijidamka, wakavaa nguo zao nzuri na kuanza safari kuelekea Kalenga… (kur. 29-35).

Utafiti uliofanyika unaendelea kudhihirisha uvumilivu alio nao Chulu mara baada ya kuokolewa na dada yake kutoka katika mikono ya maadui (Wadachi). Hali aliyomkuta nayo inaonesha kuwa ameadhibiwa sana na maadui hao. Kwa hiyo, baada ya kuondoka pale, Chulu anajisikia maumivu makali sana lakini anavumilia kwani anaona bora hayo maumivu kuliko kuendelea kuwa mikononi mwa maadui. Hili linajidhihirisha mwandishi anaposema:

> Sasa ikabakia kuondoka mahali pale bila kuonekana. Hawangeweza kuongea wala kushauriana. Mbumi aligeuka na kuanza kuondoka taratibu, akitembea kwa mikono na miguu. Chulu alimfuata nyuma kwa mwendo huohuo wa nyatunyatu. Mikono na miguu yake ilikuwa imekufa ganzi, lakini alijikaza. Maungo yalikuwa yanamuuma na kichwa kinamuwanga kutokana na kipigo alichokipata jioni ile kutoka kwa watekaji wake, lakini alivumilia. Alifurahi kuponyoka mahali pale pa hatari (uk. 87).

Huu ni uvumilivu wa hali ya juu kutembea kwa siku sita katika misitu na vichaka vikubwa, milima na mabonde yenye baridi na umande mwingi, kuumwa sana na kichwa na maumivu ya mwili. Nafsi ya kiwango cha kati inamsukuma kuvumilia ili matamanio yake ya kutoka katika mikono ya watekaji yaweze kutimia.

Tatu, ni wepesi wa kuomba msamaha pale wanapokosea. Kwa kuwa watu hawa wanapenda sana suluhu na amani itawale, wanakuwa wepesi sana kuomba msamaha. Mara zote Chulu anapogundua kuwa amemkosea dada yake kwa kumdharau, anaomba msamaha ili waendelee na mapambano dhidi ya maadui. Mwandishi anasema:

> "Mimi sitashangaa kama tukikutana nao," Mbumi alitamka. "Ila tuna ujumbe muhimu kwenda kwa Mundewa. Wakitukamata ndio mwisho wa safari."
>
> "Safari ya masafa au safari ya maisha?" Chulu alimhoji.
>
> "Zote."
>
> "Kukamatwa si rahisi," Chulu alisema kwa kujiamini. "Hasa sisi wanaume…"
>
> "Lakini inaweza kutokea," Mpunza alitahadharisha.
>
> "Kwa hiyo mimi mwanamke ndiye nitakamatwa, siyo? Wewe Chulu vipi?"
>
> "Samahani dada, nilikuwa natania tu."
>
> Mbumi aliendelea, "Ikibidi afadhali tufe kuliko kufichua siri ya nchi." (kur. 51-52).

Mbumi hapendi kudharauliwa, na Chulu anaomba msamaha mara anapogundua amemkosea dada yake. Utashi wake ndio unaomsukuma kuomba msamaha. Kwa kuwa Mbumi hana kisirani, anamsamehe na jambo hilo linaishia hapohapo. Mtafiti anaona kuwa jambo analolifanya Chulu ni la busara kubwa kwani wapo katika mapambano,

hawatakiwi kukatishana tamaa kwa namna yoyote. Pia, imebainika kuwa kutofautiana silika zao kumewasaidia kufanya kazi kwa pamoja bila kukwazana kwa kiasi kikubwa.

Sifa ya nne ni kupenda kujitolea kwa shida za wengine. Sifa hii imebainika kwa Chulu ambaye anajitolea kufa na kupona kuitetea nchi yake. Pamoja na umri alio nao, haoneshi woga hata pale wanapopewa maagizo mazito na viongozi mbalimbali. Kwa mfano, baada ya kufika nyumbani kwa Mundewa (Mtemi wa kijiji cha Kwailoza (Kilosa)) na kuripoti katika kikosi cha Wanasokomoko, Chulu na Mbumi wanaambiwa kuwa wanaitwa Ikulu kwa Mundewa. Wanapofika anawapa maagizo aliyowaitia, nao wanakubaliana naye kwa mustakabali wa nchi yao. Mundewa anasema:

> Tumewaiteni ninyi kwa sababu tunafikiri, baada ya safari yenu ya Bagamoyo, mnao uzoefu wa kutosha kuliko wanasokomoko wengine. Aidha yule Mutandisi kwa matakwa ya mahoka aliwakabidhi mikoba. Waaidha, Mwanyenza, mjumbe wa Mutwa, bado anaumwa sana, hawezi kufuatana nanyi. Itabidi aendelee na matibabu. Nyinyi bado ni watoto wadogo lakini wenye upeo na uzoefu wa kiutu-uzima… “Sisi tupo tayari kutekeleza yote unayotaka, Mheshimiwa,” Chulu alisema (uk. 21).

Chulu anaweza kuchunguza uadilifu wa tendo, wema na ubaya wake kabla ya kulitenda. Muda wote anakuwa na utayari wa kupambana na maadui licha ya umri wake kuwa mdogo.

Hata hivyo, Chulu ameonesha udhaifu kwa kusawiriwa kama mwoga wa kuanzisha jambo. Utafiti ulibaini kuwa ijapokuwa anaogopa kuanzisha jambo lakini likishaanzishwa hulifanya kwa umakini. Mathalani, hata baada ya kusikia vishindo nje ya nyumba yao anaendelea kubaki kitandani akisubiri kama kuna mtu atatoka ili naye atoke. Katika mazingira ya kawaida imezoeleka kuwa watoto wa kiume huwa jasiri ukilinganisha na wa kike. Chulu anasukumwa na nafsi ya kiwango cha msingi kuendelea kubaki kitandani hadi anaposikia dada yake anatoka. Mwandishi anafafanua hili kwa kusema:

> Mbumi alianza kutembea gizani kuelekea mlangoni. Hajafika kizingitini akasikia Chulu akiita, “Bibi!”
> “Siyo bibi, ni mimi Mbumi,” dada yake aliitikia.
> “Umevisikia hivyo vishindo?”
> “Ndiyo; nakwenda kuangalia.”
> Alimsikia Chulu akiteremka kitandani. Punde wote wawili walikuwa mlangoni. Chulu alikuwa ameshika mkuki aliouacha marehemu baba yake. Mbumi alizoa mundu hapo sebuleni, akaukamata imara kwa mkono wa kulia (uk. 5).

Kwa hiyo, matendo yote anayoyafanya Chulu ni ithibati ya silika yake ambayo inamtofautisha na Mbumi. Pia, kupitia matendo hayo imetusaidia kujua silika yake ambayo ni melankoli.

### 5.2 Silika ya Mbumi

Katika utafiti uliofanyika, imebainika kuwa Mbumi amesawiriwa mwenye sifa na matendo yanayomuweka katika silika ya koleriki. Silika hii ni ya watu ambao hisia zao zipo nje lakini hutofautiana na sangwini kwani wao zipo nje kwa kiasi kikubwa sana. Kama tulivyotangulia kubainisha katika kuelezea sifa za kila silika ni kwamba hakuna mtu mwenye silika moja bali tunaangalia ipi inajitokeza zaidi. Sifa zinazomuweka Mbumi katika kundi hili kwa mujibu wa utafiti uliofanyika ni hizi zifuatazo: kwanza ni ujasiri katika mambo anayoyafanya na hana woga. Riwaya nyingi humsawiri mwanamke au mtoto wa kike kuwa ni kiumbe dhaifu na asiye na maamuzi bali huamuliwa kila kitu na mwanamume. Mathalani, Moh'd (2017) akichunguza riwaya ya *Utengano* anaeleza kuwa mwanamke amesawiriwa kama mtawa. Ametoa mfano wa Maimuna anayetawishwa na baba yake mzee Maksuud na kunyimwa haki na uhuru. Tofauti na riwaya nyingine, katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* mwanamke amepewa sifa za ujasiri ambazo wakati mwingine huwashinda hata wanaume. Utafiti umebaini kuwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya hii, Mbumi ameonekana ni jasiri asiyekata tamaa. Mwanzoni mwa hadithi mwandishi anatanabahisha ujasiri wa Mbumi kwa kusema:

> Mbumi alianza kutembea gizani kuelekea mlangoni. Hajafika kizingitini akasikia Chulu akiita, "Bibi!" "Sio bibi, ni mimi Mbumi," dada yake aliitikia. "Umevisikia hivyo vishindo?" "Ndiyo; nakwenda kuangalia." Alimsikia Chulu akiteremka kitandani. Punde wote wawili walikuwa mlangoni. Chulu alikuwa ameshika mkuki aliouacha baba yake. Mbumi alizoa mundu hapo sebuleni, akaukamata imara kwa mkono wa kulia. Walitoka nje. Kulikuwa bado hakujapambazuka, japo dalili za wekundu wa mapambazuko zilikuwa zinaanza kuonekana mbali sana mashariki (uk. 7).

Hapa mwandishi anatuonesha ujasiri alionao Mbumi kwamba baada ya kusikia vishindo bila woga anaamua kutoka nje kwenda kuangalia nini kinatokea. Nafsi ya Mbumi inafanya maamuzi ya busara kutoka nje kulingana na msingi wa tatu wa nadharia. Pacha wake anasikia lakini bado yupo kitandani, huenda anaogopa kutoka peke yake.

Mwandishi anazidi kufafanua ujasiri wa Mbumi pale anapokaa mianzini na Chulu kumsubiri Mpunza ambaye alikwenda kwa Munzagila (baba yake Mpunza ambaye ni jumbe wa kijiji), Iringa kupeleka habari juu ya kuonekana kwa maadui. Baada ya kupata chakula wanajipumzisha mianzini. Mbumi haridhishwi na hali hii ya kukaa ilhali wao ni vijana na wametumwa kuitumikia nchi yao. Mtafiti amebaini kuwa pamoja na giza lililopo nje na mazingira ya pori, Mbumi haoni tabu kwa sababu ya ujasiri alio nao. Chulu anafuata tu kile asemacho pacha wake lakini endapo asingesema huenda angeendelea kupumzika na wasingejua wapi walipo maadui na kile wanachokifanya. Hivyo basi, anaamua kutoa wazo la kijasiri;

> "Kwa nini tunaketi hapa kama mitungi?"
> "Unataka tufanye nini?" Chulu alimjibu.
> "Tunakuwa kama si wanasokomoko?"

> "Eh?"
> "Kwa nini tusitoke hapa mianzini tukaenda huko kilimani kuangalia adui anafanya nini?"
> "Ni wazo zuri Chulu alimwitikia." Waliondoka taratibu, kimyakimya, mle mianzini… walinyatianyatia kimyakimya, wakavuka kijito cha Lugalo, wakaanza kupanda kilima ng'ambo ya pili kuelekea kule walikowaona maadui alasiri ile. Walipanda kwa taabu kizani, mara kwa mara walijikwaa kwenye majabali au kukwaruzwa na vichaka vyenye miiba… (uk. 63).

Sehemu nyingine inayoonesha ujasiri wa Mbumi ni pale ambapo Chulu anakutana na adui na kumuamrisha asimame. Masimulizi yanabainisha kuwa Chulu hasimami ila anakimbia kurudi juu ya kilima walipokuwa na dada yake kabla. Anapofika anamwamuru dada yake akimbie ili asikamatwe na adui, anamrushia Mkuu-wa Mianzi, Mbumi anaudaka. Pamoja na kusisitizwa na kaka yake kukimbia, Mbumi hakimbii. Utafiti uliofanyika uliona kuwa Mbumi alifanya hivyo kutokana na silika yake. Mwandishi anasema:

> Mbumi hakukimbia. Aliinama ghafla, akaokota jiwe kubwa, akalitupa kwa nguvu zake zote kuelekea kule alikokuwa adui. Hakujua kama jiwe hilo litampata mtu huyo au la, ila alisikia kishindo cha mtu aliyeanguka. Kisha pakawa kimya. Alianza kukimbia kuelekea upande wao huku akimhimiza Chulu, "Twende! Twende haraka!"(kur. 64-65).

Kutokimbia kwa Mbumi na kudiriki kurusha jiwe tumeona kuwa ni ujasiri mkubwa. Kama angekuwa goigoi angeweza kutimua mbio ili kuokoa roho yake. Chulu pamoja na kumuhimiza dada yake akimbie anakamatwa kwa sababu alipunguza mwendo baada ya kuona kimya kimetawala akijua kuwa adui yule ameshauawa kumbe jiwe la Mbumi lilimpata tu jichoni, hivyo, kumuongezea hasira zaidi. Matukio yote baada ya Chulu kukamatwa yanadhihirisha ushujaa alio nao Mbumi. Hakukaa chini na kuanza kulia bali alikimbia peke yake ili apeleke taarifa kwa Munzagila kuhusu kukamatwa kwa Chulu.

Hata hivyo, tukio la Chulu kukamatwa linazidisha ujasiri wa Mbumi kwani anajihisi kuwa ni mtu anayetegemewa na ndugu yake pamoja na nchi yake. Ari ya kumkomboa ndugu yake inaongezeka ingawa ameshatoa taarifa kwa Munzagila na kuahidiwa kuwa Chulu atapatikana tena akiwa salama salimini. Hivyo, usiku huo alitoroka ili kutimiza azma yake ya kumuokoa pacha wake. Masimulizi yanabainisha kuwa anapotoka nje kiza ki totoro lakini hajali. Macho hayana msaada kwake, hivyo anatumia zaidi masikio. Anasikia sauti za wadudu na wanyama tu. Anaendelea na safari yake kwa kupanda na kuteremka kwenye vilima, na mara chache anajikwaa lakini hakukata tamaa. Anapofika katika mianzi, anaingia ili atafakari namna ya kumuokoa Chulu. Maisha yanamkuza ingawa bado ni mdogo kiumri. Mwandishi anafafanua:

> Mbumi aliulaza Mkuu-wa-Mianzi mapajani kwake, akakishikilia barabara kisu chake, akaketi vizuri huku amejiegemeza kwenye mwanzi

> mnene na kuwaza juu ya maisha na mapambano na mauti. Wakati huu hakuwa kigori wala mtoto tena; alikuwa yu mtu mzima, askari mkali, mjanja na jasiri. Alikuwa Mwanasokomoko. Hakuogopa kifo (kur. 78-80).

Mbumi anajitahidi kutumia mbinu mbalimbali ili kukidhi matamanio yake ya kumuokoa pacha wake. Mathalani, anatoa mlio kama paka mwitu ambao walifundishwa katika mafunzo ya Wanasokomoko ili kumwarifu Chulu kuwa anakuja kumuokoa. Kutokana na ujasiri alionao anaanza kutembea miongoni mwa maadui. Mwandishi anasema:

> Mbumi alianza kutembea taratibu miongoni mwa maadui waliolala kwa miguu na mikono kama chui kwenye mawindo, akimkagua kila askari. Alipoona askari huyo amejitingisha alitulia kimya kama maiti. Askari huyo alifumbua macho na kumuona Mbumi. Hakushtuka; alijua kuwa katika msafara wao walikuwamo wanawake na wasichana kadha, maana askari Waafrika waliruhusiwa kwenda vitani na wenzi wao iwapo walitaka. Mbumi alisubiri hadi askari huyo arejee usingizini kabla ya kuendelea na ukaguzi wake (uk. 84).

Mtafiti anaona kuwa kitendo cha Mbumi kutembea miongoni mwa maadui ni watu wachache wanakiweza ambao wamejitoa mhanga kwelikweli. Mbumi anafanya yote hayo ili kukidhi matamanio ya kumuokoa ndugu yake. Katika mazingira kama hayo ni hatari kwa sababu kutokana na giza angeweza kumkanyaga askari yeyote akashtuka na kumgundua hivyo angebainika kwa maadui.

Sehemu nyingine inayosawiri ujasiri wa Mbumi ni pale wanapowaona maadui wanakuja upande wao wakati vita vinaendelea. Chulu anaonesha kushtuka na kumshauri dada yake wakimbie. Kutokana na silika yake, Mbumi hakubaliani na wazo la Chulu kwani kukimbia haikuwa sahihi kwa kuwa kwa wakati huo watu wote walikuwa wakipigana. Mtafiti amebaini kuwa Chulu ana wasiwasi na hivyo anamuuliza dada yake nini cha kutafanya. Mbumi anatoa ushauri wa kijasiri kwa kusema:

> “Twendeni kule juu kilimani tukawasaidie wenzetu.” Mbumi aliongoza njia kupitia mianzini na vichakani bila kuonekana, hadi wakakizunguka kile kilima mpaka upande wa pili kulikokuwa na askari wengi kiasi. Mbumi alianza kupanda kilima huku Chulu akimfuata. Walifika juu ya kilima ambapo palikuwa na chungu kubwa ya mawe. Mbumi alisogelea chungu hiyo ya mawe, akachagua jiwe moja na kulisukuma kwa nguvu zake zote kuelekea kule walikokuwako maadui. Jiwe hilo lilibiringika kama mpira kwenye mteremko mkali wa kilima, likijigonga kwenye majabali na kuruka juu ya vichaka kwa mvumo na vishindo. Kabla halijafika chini ya kilima Mbumi alikuwa ameshaporomosha mawe mengine kama matano, yakawa yanafuatana kwa vishindo mithili ya vipande vya jabali lililolipuliwa kwa baruti (uk 104).

Mwandishi anasimulia kuwa wakati Mbumi anafanya yote haya Chulu alikuwa akimtazama na kushangaa vitimbwi vya dada yake lakini alipomuelewa ilibidi aungane

naye na kumsifu kuwa ana akili sana. Mbumi anamtahadharisha ndugu yake asisimame sana ili maadui wasimuone. Mtafiti anaona kuwa kitendo hiki cha Mbumi ni cha kijasiri sana ukilinganisha na umri alio nao kwani ana uwezo wa kukimbia kama kaka yake alivyomshauri awali. Kutokana na msingi wa pili wa nadharia, Mbumi hakimbii kwa sababu anataka kukidhi haja ya matamanio yake ya kupambana kuiokoa jamii yake na nchi kwa ujumla.

Sifa nyingine iliyobainika ni kuwa na maamuzi. Watu wa silika ya koleriki wana maamuzi ya haraka na sahihi; mara nyingi wanapofanya maamuzi hayo hawakosei. Utafiti ulibaini kuwa Mbumi ni mtu wa maamuzi na mara zote anapoamua kinachofuata ni utekelezaji tu. Baada ya kusikia vishindo nje ya nyumba yao Mbumi anazinduka kutoka usingizini na kuketi kitandani. Maamuzi ya awali kufanya ni kumuamsha bibi yake. Mwandishi anasema:

> Hakukawia zaidi. Aliruka kutoka kitandani, akamshika bibi na kumtikisa huku akisema kwa sauti ndogo, “Bibi amka! Kuna radi.” Bibi aliamka na kuketi kitandani, akauliza kwa sauti ya usingizi, “Radi gani?” “Nasikia mishindo; labda kuna tufani yenye ngurumo!” Hakutaka kumweleza bibi kuwa alikuwa amesikia mishindo ya bunduki. “Kuna nini?” Bibi alimaka huku akijizoazoa kitandani. Alisikiliza. “Labda ni vita! La haula! Mahoka wapishe mbali! Mateso tuliyopata hayajatosha tu?” Bibi, ambaye sasa alikuwa yu macho kabisa, alilalama huku akirusha mikono yake iliyokaza misuli (uk. 4).

Kutokana na nukuu hapo juu, ni dhahiri kwamba maamuzi ya Mbumi ni sahihi kwani kama angemuacha bibi huenda angekuja kujilaumu baadaye au lolote lingeweza kumtokea. Nafsi ya kiwango cha ukomavu inamsukuma kufanya hayo baada ya kuchunguza wema na ubaya wa kumuamsha bibi yake. Kwa hiyo, Mbumi anapoona bibi ameamka kabisa anafanya maamuzi ya kutoka nje kwenda kushuhudia nini kinachotokea.

Maamuzi mengine anayoyafanya ni kwenda kutoa taarifa kwa Munzagila juu ya kukamatwa kwa Chulu. Mbumi anafahamu kuwa maisha ya ndugu yake yapo hatarini na yanamtegemea yeye, hivyo, haoni sababu yoyote ya kupoteza muda. Mbumi anaendelea kukimbia akiwa peke yake hadi anapofika kijiji cha Viwengi na kuoneshwa nyumbani kwa Munzagila kisha akatimiza azma yake ya kuwaarifu kuhusu kukamatwa kwa Chulu na wageni aliowaona. Matamanio yake ni kumuokoa ndugu yake ili waendelee na mapambano na kutimiza haja yake ya kuwakomboa Wasagara na nchi kwa ujumla. Mwandishi anatanabahisha:

> Aliteremka kilima mbio mbio, akaacha njia ya kushoto ya kurejea mianzini, akafuata njia ya kulia iliyoelekea kijiji cha Viwengi ambacho alihisi kilikuwa karibu. Hapakuwa na wasaa wa kupitia tena mianzini kuchukua mizigo yao. Potelea mbali! Vitu walivyoviacha huko vitafuatwa baadaye hatari ikishapita. Alikaza mwendo. Ingawa baridi ilikuwa kali, lakini jasho lilikuwa likimtoka mwili wote. Alikuwa akihema, lakini dharura ile ilimfanya asihisi uchovu. Kichwani alikuwa akiwafikiria watu wale aliowaona… (uk. 66).

Si hayo tu, imebainika pia maamuzi mengine anayoyafanya Mbumi ni kutoroka nyumbani kwa Munzagila alipokuwa amekaribishwa. Mbumi anatakiwa kulala ili siku inayofuata Munzagila awatume vijana wake kumtafuta Chulu. Lakini, wazo lake ni moja tu; kumkomboa ndugu yake kutoka katika mikono ya maadui. Dhamiri yake muda wote inamwambia kuwa hatima ya uhai wa Chulu na nchi yake kwa ujumla vipo mikononi mwake. Nafsi ya kiwango cha kati inamuongoza kutoroka kwa kuona kuwa Munzagila anachelewa. Hivyo, hajali lolote katika kutimiza azma hiyo. Mwandishi anafafanua:

> Baada ya kula Mbumi akiwa na Mkuu-wa-Mianzi alitoka nje bila kuaga. Aliwapita kwa taabu, akichelea kuwakanyaga, wasichana na wanawake waliokuwa wamelala ndani na nje ya nyumba. Nje ya uzio alikuta wanaume wengi wenye silaha wameketi wakisubiri amri ya kwenda Lugalo kupambana na maadui. Aliwapita kwa mbali gizani, akaingia kwenye njia kuu na kuanza kupiga mbio kuelekea Lugalo (uk. 77).

Mbumi anafanikiwa kukimbia katika usiku wa giza nene kiasi kwamba hata anapoona visiki na vichaka anahisi kuwa ni mazimwi au wanyama wakali. Mwandishi anasema kuwa mara kwa mara anajikwaa, anaanguka na kuinuka tena lakini hajali kwa sababu nia yake ni moja tu. Hatimaye anafika sehemu aliyotarajia na kutimiza azma yake ya kumuokoa nduguye.

Maamuzi mengine anayoyafanya ni katika ukurasa wa 104 baada ya kuona maadui wanaelekea upande wao hakimbii. Anamwambia ndugu yake wapigane kufa na kupona na anapanda kilimani na kuanza kuporomosha mawe kuelekea upande walipo maadui. Jambo ambalo linafanikiwa kwani mawe yale yaliwapiga na kwachanganya sana maadui wakawa wanakimbia na kurusha risasi ovyo.

Sifa nyingine ya koleriki ni kutopenda kudharauliwa. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, Mbumi hapendi kudharauliwa na mtu yeyote bila kujali umri wala jinsia. Kutokana na udogo wake na jinsia yake watu wengi wanamdharau kwa kumuona hawezi kufanya kitu. Jambo hili linamuudhi sana na hasiti kulikemea kila linapotokea. Kwa mfano, baada ya kufika kwa Mutwa, Mbumi na Chulu wanaeleza kilichowaleta. Wanaeleza kwa kupokezana lakini maelezo ya ufasaha ya Mbumi yanawashangaza wengi; hawakutegemea binti kama yeye angeweza kutoa maelezo hayo. Mwandishi anasema:

> Mutwa aliuliza maswali machache ambayo yalijibiwa na Mbumi na Chulu kadiri walivyoweza. Maswali hayo zaidi yalihusu hali ya maadui, silaha zao na mipango ya mapambano ya wana-Kwailoza. Majibu ya ufasaha ya Mbumi yalifanya baraza zima limkodolee macho kwa mshangao. Hatimaye mzee mmoja aliuliza, "Wewe binti unajuaje mambo hayo? Wewe ni askari? Umepigana vita?" "Nimeona na nimepigana," Mbumi alijibu kwa ufupi. "Kweli enzi mpya zaja," yule mzee aliongezea. "Tayari zimeanza," Mbumi alijibu "ndiyo maana tupo hapa"(uk. 43).

Katika nukuu hii, mzee huyo anamdharau Mbumi kutokana na usichana wake na udogo wake lakini Mbumi anampa majibu yenye uhakika yanayomshangaza. Katika

mazingira ya kawaida watu hususani wanaume huwadharau sana watoto wa kike kwa kuona kuwa hawajiwezi. Pia, wanajiaminisha kuwa kila kitu lazima wasemewe na wanaume kitu ambacho mwandishi ameendelea kutufungua macho na kutuonesha kuwa siyo kweli.

Kwa upande mwingine, imebainika kuwa Chulu naye anaonesha dharau kwa dada yake kutokana na kuwa msichana. Chulu anaamini kuwa si rahisi kwa mwanamume kukamatwa lakini mwanamke anaweza kukamatwa na maadui. Chulu analiamini hili kutokana na mfumo dume ambao anauishi. Haya yalitokea wakati wakijadiliana na Mpunza kuhusu kukutana na maadui. Mwandishi anafafanua:

> "Mimi sitashangaa kama tukikutana nao," Mbumi alitamka. "Ila tuna ujumbe muhimu kwenda kwa Mundewa. Wakitukamata ndio mwisho wa safari."
> "Safari ya masafa au safari ya maisha?" Chulu alimhoji.
> "Zote."
> "Kukamatwa si rahisi," Chulu alisema kwa kujiamini. "Hasa sisi wanaume…"
> "Lakini inaweza kutokea," Mpunza alitahadharisha.
> "Kwa hiyo mimi mwanamke ndiye nitakamatwa, siyo? Wewe Chulu vipi?"
> "Samahani dada, nilikuwa natania tu."
> Mbumi aliendelea, "Ikibidi afadhali tufe kuliko kufichua siri ya nchi" (kur. 51-52).

Kwa mujibu wa nukuu hiyo, mawazo ya Mbumi yalikuwa sahihi kwani hata Mpunza ambaye aliwazidi umri anashadidia kwamba katika hali kama ile lolote linaweza kutokea bila kujali jinsia ya mtu.

Sehemu nyingine inayoonesha Mbumi anachukia kudharauliwa ni pale wanapokutana na askari wa doria ambaye anawakamata akijua ni maadui. Bahati nzuri Mpunza anajitokeza akiwa na sauti ya furaha akitokea kwenye doria ya upande mwingine. Yule askari anawaachia baada ya kugundua ni wenzao lakini anawaonya. Mwandishi anasema:

> "Nisiwaone upande huu tena, watoto; kuanzia sasa huu ni uwanja wa mapambano," yule askari mrefu alisema.
> "Hakuna watoto hapa." Mbumi alimwitikia.
> "Kumbe," yule askari alifoka. "Naona mna midomo! Si kosa lenu; hamjui msemalo wala mtendalo!" Alimalizia na kutema mate chini kwa hasira.
> "Tunajua kuwa mapambano tumeshayaanza sisi!" Mbumi alimwarifu. "Twendeni!" waliongozana na Mpunza kuelekea mianzini (uk. 90).

Mbumi anachukia kuitwa mtoto, anaona ni dharau kubwa kwa kuwa hata wao wamekuja kwa ajili ya kupambana ili kuikomboa nchi yao. Nafsi ya kiwango cha kati inamuongoza Mbumi kujua kipi ni kibaya na kipi ni kizuri. Kuitwa mtoto ilhali amekwenda kupambana anaona ni kitu kibaya sana. Pia, kitendo cha askari kufoka na

kutema mate chini ni dharau kubwa sana kwake. Mbumi anaonesha kukichukia kitendo kile na kukikemea. Mtafiti alipofanya mahojiano na Mulokozi (2020) alisema kuwa kuingiliana kwa misukumo ya kijamii na kiutamaduni husababisha kijana kuwa shujaa hata kama hajafikia umri wa utu uzima.[4]

Sifa nyingine ya watu wa kundi hili ni kuvutiwa sana na mazingira na kupanga vitu kwa unadhifu. Imebainika kuwa katika safari yao ya kuelekea kwa Mutwa Mukwava wanapita maeneo mengi na wanavutiwa sana na mazingira hayo. Kwa mfano, masimulizi yanaeleza kuwa wanavutiwa sana na mianzi wanayoiona. Ni mingi sana ya kijani na ya manjano ikipepea taratibu katika upepo mwanana wa asubuhi. Mianzi hiyo ni mirefu, yenye afya, yenye majani mazuri ya kijani yanayochezacheza kufuata mwendo wa upepo. Mandhari hayo yanavutia sana mpaka yanasababisha Mbumi amake kwa mshangao:

> "Chulu unaiona hiyo ngoma ya mianzi?" "Ngoma?" Chulu aliuliza kwa mshangao. "Siioni." "Huioni hiyo mianzi inavyocheza vizuri kwa madaha? Utadhani ngoma yetu ya rika ya dighubi?" Chulu ambaye hakuwa makini kwa uchunguzi kama mwenzake, sasa aliitazama mianzi hiyo kwa kituo na kusema bila kumtazama mwenzie, "Kweli inapendeza. Utadhani mkwajungoma!" (kur. 32-33).

Kwa hiyo, pamoja na kuwa wote wanaiona mianzi, Mbumi anakuwa wa kwanza kuvutiwa na jinsi inavyocheza kwa sababu ya silika yake.

Mazingira mengine yanayobainishwa kumvutia Mbumi ni katika ngome ya Lipuli. Katika safari yao baada ya kuvuka vilima kadhaa, wanafika juu ya safu ya milima iliyozunguka mbuga pana sana ya kipenyo cha zaidi ya kilomita kumi. Munzagila anawahabarisha kuwa hiyo ni ngome ya Lipuli au Kalenga. Mwandishi anafafanua namna ngome hiyo ilivyokuwa:

> Kutoka pale walipokuwa waliweza kuiona vizuri hiyo Lipuli au ngome ya Kalenga. Waliona kuwa Kalenga ilikuwa mji mkubwa ulioshikamana vizuri na kuzungushiwa kuta mbili: ukuta wa nje ulijengwa kwa magogo yenye miiba na ambao muda wote ulikuwa ukilindwa na mamia ya askari wenye mikuki na magobori; na ukuta wa ndani uliokuwa umejengwa kwa mawe makubwa… Kwa muda Chulu, Mbumi na Mpunza walisimama kilimani wakiyafurahia na kuyastaajabia mandhari yale ya Kalenga. Punde Munzagila aliwaashiria waendelee na safari. Waliteremka kwa haraka kuelekea chini mbugani (kur. 36-37).

Sehemu nyingine inayoonesha kuwa Mbumi anavutiwa sana na mazingira ni kwenye bonde la Lugalo, ambalo limefunikwa na majani mengi marefu ya aina ya matete na mabingubingu yaliyokuwa yakipepea taratibu kufuata upepo. Mwandishi anasema:

---

[4] Mahojiano baina ya mtafiti na Profesa Mulokozi yalifanyika Februari 20, 2020 katika ofisi yake iliyopo katika jengo la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mulokozi ni Profesa mstaafu ambaye alikuwa akifundisha katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, ni mwandishi wa kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili.

> Walisimama kwa muda mrefu wakiangalia bonde hilo pana la Lugalo. Walivutiwa na upana na utulivu wake. Walivutiwa na vijia vya miguu vilivyoteremkia humo bondeni kutoka ng'ambo zote mbili. Walivutiwa na vichaka vyeusi vilivyofunika magenge na miteremko iliyoizunguka bonde hilo; walivutiwa pia na nyasi ndefu na matete yaliyofunika kingo za mto wa Lugalo uliokuwa ukitiririka taratibu huko bondeni. Kila walichokiona hapo kilivutia. Hata ndege wa angani… Mbumi na Chulu walivutiwa na mambo yote kwasababu yalionesha ujana, uhai na matumaini (uk. 56).

Kwa hiyo, haya yote ni mazingira ambayo Mbumi yanamvutia sana. Wakati mwingine wanajisahau kama wako safarini. Hii ndio silika ya watu walio katika kundi hili. Mara nyingi wanapokuwa katika mazingira yanayowazunguka hutumia muda mwingi kuangalia mazingira hayo kutokana na kuvutia kwake.

Pia, utafiti umebaini kuwa watu wa kundi hili huweka vitu vyao katika mpangilio mzuri wakati wote. Mathalani, wanapojiandaa na safari watoto hawa wanabeba mizigo mbalimbali vikiwamo vyakula. Mbumi anajitahidi kubeba kila kitu ambacho kingehitajika njiani. Bibi yao anawaongezea vyakula zaidi lakini Mbumi anamkatalia kwa kuwa vingeongeza uzito. Hii inasimuliwa katika ukurasa wa 26 mwandishi anaposema:

> "Bibi!" Mbumi alimkatisha. "Vinatosha hivyo! Wewe utakula nini tukichukua kila kitu? Kwanza vizito, hatuwezi kuvibeba vyote. Tulivyochukua vinatosha," alimalizia huku akishindilia kapu lake, lililokuwa tayari limejaa makorokoro mengine.

Ili kuthibitisha jinsi Mbumi anavyojua kupanga vitu vyake vizuri utafiti umebaini kuwa pale wanapokuwa na haja ya kupata moto baada ya kujikuta porini na jua limezama, Mbumi hana wasiwasi kwa sababu anajua lazima moto utawaka. Baada ya kukusanya kuni Chulu anacheka sana na kumshangaa dada yake kwamba atawasha moto na nini. Haya yanabainishwa kama ifuatavyo:

> Mbumi hakusema neno. Aliinuka, akachukua kapu lake, akalifungua, akatoa kipande cha ubao kilichokuwa na tundu katikati, akakiweka mbele yake. Halafu akachukua ujiti mwembamba, akauchomeka katika kibao kile na kuanza kupekecha. Chulu alimtazama Mbumi kwa mshangao, halafu akasema kwa kufahamikiwa, "Ala, kumbe umeleta ulindi na wimbombo? Ulikumbukaje?"
> "Wewe ulifikiri kapu lote hili nimebeba nini?"
> "Manukato na mapambo tu."
> "Basi umekosea. Kila kitu kina wakati wake. Kuna wakati wa utoto na wakati wa utu uzima. Kuna wakati wa kujipamba na wakati wa kujipambua…" (kur. 30-32).

Kwa hiyo, imebainika kuwa vitu vya Mbumi vilipangwa vizuri ndiyo maana Chulu hakutegemea kuwa angeweza kubeba vitu vyote hivyo. Kwa kuwa hulka ya wanawake ni kujipamba alidhani kuwa dada yake amebeba mapambo na manukato tu.

Sifa nyingine inayomuweka katika kundi hili ni kuthubutu. Kwa mujibu wa utafiti wetu inapotokea kuna jambo hata liwe gumu kiasi gani watu wa silika hii huthubutu kulifanya na mara nyingi matokeo yake huwa chanya. Kutokana na kuthubutu, wengi huishia kuwa matajiri au kupata heshima kubwa katika jamii. Mbumi anathubutu kutoka nje anaposikia ngurumo na mishindo ya bunduki (kur. 4-5). Pia, anathubutu kuondoka bila kuaga katika boma la Munzagila ili aende kumuokoa ndugu yake ambaye alikuwa ametekwa. Mwandishi anafafanua:

> Baada ya kula Mbumi akiwa na Mkuu-wa-Mianzi alitoka nje bila kuaga. Aliwapita kwa taabu, akichelea kuwakanyaga, wasichana na wanawake waliokuwa wamelala ndani na nje ya nyumba. Nje ya uzio alikuta wanaume wengi wenye silaha wameketi wakisubiri amri ya kwenda Lugalo kupambana na maadui. Aliwapita kwa mbali gizani, akaingia kwenye njia kuu na kuanza kupiga mbio kuelekea Lugalo… (uk. 77).

Kwa hiyo, tangu mwanzo hadi mwisho, masimulizi yanaonesha kuwa Mbumi anathubutu kuipigania nchi yake kwa kupeleka ujumbe wa siri kwa Mukwava ijapokuwa safari inakuwa ndefu, yenye hatari naye ana umri mdogo.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imezungumzia uhusiano baina ya silika na utendaji wa wahusika wakuu wa fasihi ya watoto. Uhusiano huu unatarajiwa kuleta tija kubwa katika ulimwengu wa fasihi kwa sababu umeonesha mtagusano baina ya fasihi ya watoto na saikolojia. Nyuga hizi mbili zina uhusiano mkubwa; fasihi haiwezi kujitenga na nyuga nyingine katika ulimwengu wa tafiti na tahakiki. Kwa kuonesha mtagusano huo, makala imepanua taaluma ya fasihi kwa ujumla na fasihi ya watoto kwa upekee. Pia, makala hii itawasaidia watunzi wa kazi za watoto kutunga kazi kwa kuzingatia silika za watoto ambao ndio walengwa wakuu. Matokeo ya utafiti wetu yanaonesha kuwa kila mhusika ana silika yake inayopambanuliwa kwa kile anachosema na anachotenda. Mbumi ana silika ya koleriki na Chulu ana silika ya melankoli. Kila aina ina udhaifu na ubora wake na hakuna silika iliyo bora kuliko nyingine, na zote zinahitajika ili dunia iwe mahali pazuri pa kuishi. Kwa hiyo, kila mtu ni wa kipekee; hakuna watu wawili wanaofanana kwa kila kitu.

## Marejeleo

Asamoah, G. (2018). A Synoptic Account of the Four Temperaments. *Interdisciplinary Research Journal of Theology, Apologetic, Natural and Social Sciences*, 1(1&2): 67-70.

Cresswell, J.W. (2009). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches*. Los Angles: SAGE Publication.

Flaskerud, J.H. (2012). Temperament and Personality: From Galen to Dar es Salaam. *Mental Health*, 3(2): 43-47.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques* (Second edn). New Delhi: New Age International (P) Limited.

Larrimore, M.J. (2001). Substitutes for Wisdom: Kant's Practical thought and the Traditional of the Temperaments. *Journal of the History of Philosophy*, 39(2): 259-288. Iliyosomwa katika https://doi.0rg/DOI:10.1353/hph.2003.0103, tarehe 21/01/2020.
Martin, M. na Bobgan, D. (1992). *Christian and the Four Temperaments*. California: East Gate.
Mbarouk, S.S. (2009). Uchambuzi wa Riwaya ya *Kiu* kwa Kutumia Nadharia ya Saikolojia Changanuzi. *Eastern African Literary and Cultural Studies*. Iliyosomwa katika https://doi.org/10.11080/232774408.2018.1540127, tarehe 13/05/21.
Mbunda, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: East African Educational Publishers Ltd.
Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.
Moh'd, M. O. (2017). Ulinganishi wa Tabia za Wahusika Wakuu na Dhamira katika Riwaya za *Kusadikika* na *Utengano*. Tasinifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Masharti ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
Mudhihiri, M. (2019). *Hulka ya Binadamu*. Iliyosomwa katika http:www.pressreader.com, tarehe17/02/2020.
Muhando, P. na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: TPH.
Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
Mulokozi, M.M. (2018). *Ngoma ya Mianzi*. Dar es Salaam: KAUTTU.
Ponera, A.S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.
Ponera, A.S. na Kasiga, G. A. (2019). Mdhihiriko wa Kionjo cha Usangwini kwa Mhusika Willy Gamba katika Riwaya ya *Njama*. *Kioo cha Lugha*, Juz .17: 99-113.
Rothbart, M.K. (2012). Early Temperament and Psychosocial Development. *In Encyclopedia onEarly Childhood Development* (2012$^{th}$ ed, p.12). Michigan: University of Oregan.
Senkoro, F.E.M. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.
Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.